# HALMASHAURI YA MANISPAA YA KAHAMA

## MUHTASARI MPANGO NA BAJETI KWA MATUMIZI YA KAWAIDA NA MIRADI YA MAENDELEO KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022

### 1.0 UTANGULIZI

Mapendekezo haya yamezingatia mambo muhimu yafuatayo;

- Sheria ya Bajeti Na.11 ya 2015;
- Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025;
- Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano 2016/2017-2021/2022;
- Mwongozo wa Maandalizi ya Bajeti wa Mwaka 2021/22;
- Mwongozo wa maandalizi ya Bajeti ya Mishahara wa Mwaka 2021/22;
- Mpango Mkakati wa Halmashauri 2016/17 -2021/22;
- Ilani ya Uchaguzi ya CCM 2020-2025;
- Miongozo na Sera Mbalimbali za Kisekta;
- Malengo Endelevu ya Milenia (SDGs);
- Tathimini ya utekelezaji kazi wa Mwaka wa Fedha 2019/2020 na mapitio ya Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 hadi Desemba.

Taarifa ya tathmini ya Mpango na Bajeti wa Mwaka 2019/2020 na Mapitio ya Mpango na Bajeti kwa waka Fedha 2020/2021 kwa kipindi cha Julai hadi Disemba 2020.

Katika Mwaka wa Fedha 2019/2020, Halmashauri ilitegemea kukusanya na kutumia Tsh **38,981,748,470.65 na Elimu Bila Malipo Tsh. 2,939,162,456.11** kwa mchanganuo ufuatao;

**A.MAPATO**

| S/N | Shughuli | Makisio 2019/20 | Mapato Halisi | % |
|---|---|---|---|---|

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Mapato ya ndani(OC) | 2,298,433,373.20 | 2,047,016,271.70 | 89.06 |
| | Mapato ya Ndani Miradi ya Maendeleo | 3,447,680,059.80 | 3,127,886,475.58 | 90.72 |
| | Mapato ya Ndani Kingwa(CHF, NHIF, User Fee, Ada SS | 1,304,947,568.00 | 1,051,227,369.92 | 80.56 |
| | **Jumla Mapato ya Ndani** | **7,051,081,000.00** | **5,339,264,602.77** | **88.30** |
| 2 | Mishahara | 26,288,257,395.00 | 20,690,454,680.00 | 78.71 |
| 3 | Mapato ya Ruzuku | 920,824,961.71 | 872,541,480.55 | 94.76 |
| 4 | Miradi ya maendeleo | 4,721,622,113.94 | 2,549,069,417.33 | 53.99 |
| | **Jumla Ndogo** | **38,981,748,470.65** | **29,451,330,180.65** | **75.55** |
| 5 | Elimu Bila Malipo | 2,939,162,456.11 | 2,939,162,456.11 | 100 |
| | **Jumla Kuu** | **41,920,910,926.77** | **32,390,492,636.76** | **77.25** |

**B. MATUMIZI**

| S/N | Shughuli | Makisio 2019/20 | Matumizi | % |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Mapato ya ndani(OC) | 2,298,433,373.20 | 2,043,700,232.96 | 80.3 |
| | Mapato ya Ndani Miradi ya Maendeleo | 3,447,680,059.80 | 2,911,912,732.45 | 91 |
| | Mapato ya Ndani Kingwa(CHF, NHIF, User Fee | 1,304,947,568.00 | 906,519,763.30 | 72 |
| | **Jumla Mapato ya Ndani** | **7,051,081,000.00** | **5,251,264,602.77** | **84** |
| 2 | Mishahara | 26,288,257,395.00 | 19,028,337,222.18 | 72.38 |
| 3 | Matumizi ya Ruzuku | 920,824,961.71 | 841,361,511.74 | 91.37 |
| | Miradi ya Maendeleo Ruzuku | 4,721,622,113.94 | 1,945,005,189.53 | 41.19 |
| | **Jumla Ndogo** | **38,981,748,470.65** | **21,814,703,923.45** | **55.96** |
| 4 | Bakaa 2017/18 | 455,916,847.95 | 434,462,224.41 | 95.29 |
| 5 | Elimu Bila Malipo | 2,939,162,456.11 | 2,939,162,456.11 | 100 |
| | **Jumla Kuu** | **42,376,827,774.71** | **25,188,328,603.97** | **59.44** |

Vipaumbele katika mwaka wa fedha 2019/20 vilikuwa katika sekta ya Elimu Msingi na Sekondari katika ujenzi wa madarasa na utengenezaji wa madawati na ukamilishaji wa miradi viporo ambayo ilianzishwa kwa nguvu za wananchi. Katika mwaka wa fedha 2019/2020, Halmashauri ilipanga kutekeleza na kusimamia shughuli za miradi ya maendeleo yenye thamani ya Tshs. 4, 721, 622,113.94 za Ruzuku toka Serikali kuu na Wahisani na Tsh 3,447,680,059.80 kutoka Mapato ya

Ndani. Hadi Juni 2020, Halmashauri ilipokea na kutekeleza miradi yenye thamani Tshs 2,549,069,417.33 kwa fedha za Ruzuku na Wahisani na Miradi yenye thamani ya Tshs 2,911,912,732.45 kwa fedha za Mapato ya Ndani sawa na asilimia 91 ya makisio na asilimia 85 ya utekelezaji wa miradi. Miradi iliyotekelezwa katika kipindi hiki imeambatishwa katika KIAMBATISHO "A".

**Mapitio ya Mpango na Bajeti 2020/2021 hadi Desemba**

Katika Mwaka wa Fedha 2020/2021, Halmashauri iliidhinishiwa kutumia Tsh **37,307,956,593.44** kwa mchanganuo ufuatao;

**A.Mapato**

| Na. | Shughuli | Makisio 2020/2021 | Mapato halisi Hadi Desemba 2020 | % |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Mapato ya ndani- HQ | 2,199,209,200.00 | 1,006,697,613.50 | 43.80 |
| | Mapato ya Ndani Miradi ya Maendeleo | 3,298,813,800.00 | 1,602,950,000.00 | 46.49 |
| | Mapato ya Ndani Lindwa (CHF, NHIF, User Fee & Ada) | 1,490,490,417.00 | 627,213,395.80 | 61.13 |
| | **Jumla Mapato ya Ndani** | **6,988,513,417.00** | **3,236,861,009.30** | **47.80** |
| 2 | Mishahara | 23,589,858,890 | 10,919,769,365.30 | 48.99 |
| 3 | Matumizi mengineyo | 1,168,559,000 | 505,275,520.00 | 55.45 |
| 4 | Miradi ya maendeleo | 2,911,517,218 | 339,266,869.89 | 11.41 |
| 5 | Bakaa | 1,221,322,122 | 616,098,109.00 | 100 |
| | **Jumla Bila Wahisani na Elimu Bila Malipo** | **35,879,770,647** | **15,001,172,764.34** | **45.53** |
| | Miradi ya Maendeleo Wahisani | 2,257,772,110.11 | 434,972,120.92 | 19.27 |
| | Elimu Bila Malipo | 1,485,663,000.00 | 179,671,048.29 | 12.09 |
| | **Jumla Kuu** | **37,307,956,593.44** | **16,231,914,042.55** | **43.51** |

**Fedha zilizopokelewa nje ya Bajeti**

| NA | CHANZO | FEDHA KISIWA | FEDHA POKELEWA | ASILIMIA |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Fedha za Chanjo | 39,827,486.00 | 2,298,453,373.27 | 34.8 |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 2 | Fedha za Uchaguzi | 290,414,888.00 | 3,447,680,059.41 | 30.9 |

**B.Matumizi**

| S/N | Shughuli | Makisio 2020/2021 | Matumizi hadi Desemba 2020 | % |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Mapato ya ndani- HQ | 2,199,209,200.00 | 886,067,560.80 | 38.6 |
| | Mapato ya Ndani Vyanzo Lindwa | 1,510,490,417.00 | 588,165,673.36 | 57.3 |
| | Mapato ya Ndani Miradi ya Maendeleo | 3,298,813,800 00 | 1,115,529,126.14 | 32.4 |
| | **Jumla Mapato ya Ndani** | **6,772,133,430.00** | **2,589,762,360.30** | **38.24** |
| 2 | Mishahara | 23,589,858,890.00 | 10,919,769,365.15 | 49 |
| 3 | Matumizi mengineyo | 1,168,559,000.00 | 511,911,938.04 | 56.2 |
| 4 | Miradi ya maendeleo S/Kuu | 2,911,517,218.00 | 314,757,864.80 | 10.6 |
| 5 | Wahisani na Elimu Bila Malipo | 1,485,663,000.00 | 548,658,972.22 | 14.7 |
| 6 | Bakaa 2019/20 | 1,221,322,122.00 | 143,213,554.77 | 23.2 |
| | **Jumla** | **37,307,956,593.42** | **15,028,074,055.00** | **40.3** |
| 7 | Nje ya Bajeti | 330,242,374.00 | 303,092,175.98 | 91.78 |
| | **Jumla Kuu** | **37,638,198,967.42** | **15,331,166,231.00** | **41** |

Vipaumbele katika Mwaka wa Fedha 2020/2021 vipo katika sekta ya miundombinu ya Elimu msingi na Sekondari katika ujenzi wa madarasa na nyumba za walimu, ukamilishaji wa miradi viporo ambayo ilianzishwa kwa nguvu za wananchi na ukamilishaji wa miundo mbinu ya kuongeza mapato kwenye masoko, eneo la uwekezaji Bukondamoyo, maegesho ya magari makubwa Majengo. Miradi yenye thamani ya Tshs 1, 115, 529,126.14 imetekelezwa kwa fedha za Mapato ya Ndani. Miradi iliyotekelezwa na fedha za Mapato ya Ndani ni pamoja na:

- Ujenzi wa Hospitali ya Mji wa Kahama,
- Ujenzi wa choo eneo la maegesho ya Magari Makubwa Majengo,
- Ukarabati wa Soko la Kazaroho,
- Ujenzi wa Nyumba 2 za walimu S/M Ntungulu,
- Ukamilishaji wa madarasa 6 na ujenzi wa matundu 7 vya Vyoo S/M Mayila,
- Ukamilishaji wa Bweni la Wanafunzi katika shule ya Sekondari Abdulrahimu Busoka,
- Ukarabati wa nyumba za Watumishi,
- Ukamilishaji wa Mtaro wa Maji ya mvua Eneo la uwekezaji Bukondamoyo,
- Ununuzi wa Jenereta na Gari na
- Ukamilishaji wa ofisi ya Kijiji cha Mpera.

Shughuli nyingine zilizofanyika ni pamoja na Upembuzi Yakinifu, Andiko Biashara na Maandalizi ya Michoro ya Stendi ya Mbulu, utoaji wa pembejeo kwa Vijana katika kata 10 na malipo ya shughuli za uzoaji taka katika kata 12 za Mjini. Fedha za Malipo za Malipo ya papo kwa papo zimetumika katika ununuzi wa dawa, Kulipa madeni ya Xray na Mashine ya kufulia na ukarabati wa Wodi ya watoto Hospitali ya Mji.

Aidha, Halmashauri katika kipindi hiki imeanza utekelezaji wa Miradi katika Sekta za Elimu Msingi, Sekondari na Afya kupitia fedha za Jamii (CSR Buzwagi) Awamu ya Pili yenye thamani Tsh.2,448,810,000.00. Katika robo ya tatu ya Mwaka 2020/21 Halmashauri itaendelea na ukamilishaji wa madarasa 34 na ofisi 2 katika Shule za Sekondari, ukamilishaji wa madarasa 93, Ofisi 13 na matundu ya vyoo 33 katika shule za Msingi. Kupitia Fedha za Mapato ya Ndani Halmashauri itaendelea na ukarabati wa

Ofisi ya Halmashauri, Ujenzi wa Hospitali ya Mji, Ujenzi wa Soko la Sango , ukamilishaji wa S/M Mayila na uzoaji wa taka katika kata za Mjini.

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** katika Mwaka 2020/2021 Halmashauri ilitenga kiasi Tshs 574,613,343.30 kwa ajili ya Mikopo ya wanawake na vijana. Tayari Kiasi cha Tsh. 267,661,666.67 kimetengwa na kiasi cha Tsh. 199,000,000.00 kimekopeshwa kwa vikundi 68 ( Tsh. 160,000,000.00 kwa Vikundi 58- Wanawake na Tsh. 39,000,000.00 kwa vikundi vya Vijana) . Vilevile Halmashauri katika robo ya tatu ya mwaka 2019/20 imepitisha kutoa mikopo ya kiasi cha Tsh.128,500,000.00 kwa Makundi haya hivyo kufanya jumla ya Tsh. 327,500,000.00 iliyoidhinishwa kutolewa sawa na 60% ya Matakwa ya Sheria ya Mikopo. Aidha katika kpindi cha 2016/2017- 2020/2021 jumla ya Tsh. 1,287,461,000.00 zimetolewa kwenye mikopo na marejesho ni Tsh. 527,497,750.00 na kubakiwa na deni na riba la Tsh. 803,509,350.00. Katika deni hili Tsh. 736,013,600.00 zipo ndani ya muda wa marejesho wakati Tsh. 67,495,750.00 ni mikopo kichefuchefu.

## 2.0 CHANGAMOTO

Changamoto tulikutana nazo katika utekelezaji wa Bajeti ya nusu mwaka 2020/2021 ni kama ifuatavyo;-

a) **Changamoto za ukusanyaji wa mapato**

i.Upungufu wa watumishi katika Idara hususani sehemu ya Biashara kwa ajili ya kufuatilia na kusimamia utoaji wa leseni za biashara.

ii. Mwitikio mdogo wa walipa kodi mbalimbali mfano ada za taka kutokana na kutokuwa na ufahamu juu ya kulipa kodi kwa wakati na usahihi.

iii. Kupungua kwa walipa kodi ya huduma (Service levy) kutokana na hatua za kuanza kufungwa kwa mgodi wa Buzwagi ambapo Makampuni mengi yaliyokuwa yakifanya kazi mgodini yameondoka.

iv.Kutokuwepo kwa usafiri wa uhakika wakati wa ukusanyaji wa Mapato ya Ndani.

vii.Mfumo wa kukusanyia mapato (LGRCIS) kukabiliwa na chanagamoto ya kupoteza mawasiliano pamoja na kuchelewa kutoa taarifa za miala na kusababisha adha kwa walipa kodi.

viii. Udanganyifu wa takwimu za walipa kodi na ushuru.

b) **Changamoto za utekelezaji wa Bajeti**

i. Ufinyu wa Bajeti yenye kutosheleza stahiki za watumishi, uendeshaji wa ofisi na utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo.

ii. Kupungua kwa makusanyo ya Mapato ya Ndani kutokana na wafanyabishara wengi kufunga biashara na mapato ya kodi ya huduma kutoka Mgodi wa ACACIA Buzwagi.

ya kawaida na Miradi ya Maendeleo kunachelewesha utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

iii. Wananchi kutokuwa na ari ya kulipa Kodi, Ada,Tozo na Ushuru wa Halmashauri.

iv. Kutokuwepo kwa usafiri wa uhakikia wa garikwa ajili ya usimamizi na ufuatiliaji wa miradi ya Maendeleo.

v. Uelewa mdogo wa Wakuu wa Idara juu uchaguzi wa vifungu sahihi na vipaumbele vya bajeti wakati wa maandalizi ya Bajeti.

vi. Uelewa mdogo wa Wakuu wa Idara kwenye masuala ya Manunuzi.

Changamoto hizi zote zimeangaliwa katika maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Mwaka 2021/2022.

## 3.0 RASIMU YA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2021/2022

Katika Bajeti ya Mwaka 2021/2022, Vipaumbele vipo katika:

- ukusanyaji wa Mapato ya Ndani kwa kuboresha vyanzo vya mapato na ukusanyaji wa tozo mbalimbali;
- Kuboresha mazingira ya kujifunzia na kufundishia kwa kukamilisha madarasa, vyoo na nyumba za walimu, utengenezaji wa viti, meza na madawati katika Idara za Elimu Msingi na Sekondari;
- Kuboresha huduma za Afya kwa kukamlisha ujenzi wa Hospitali ya Mji, ukamilishaji wa Vituo vya Afya Nyasubi na Mwendakulima, ukamilishaji wa zahanati za Chapulwa, Wendele na Ngulu;

- Kuboresha mazingiara ya kufanyia kazi kwa kukamilisha ujenzi/ukarabati wa Ofisi Makao Makuu ya Halmashauri, Ofisi ya Kata Kilago na Busoka pamoja na ukamilishaji wa miradi Viporo.

- Aidha katika bajeti hii pia tunatarajia kutekeleza Miradi Mikakati ya kuboresha miundombinu katika eneo la uwekezaji Bukondamoyo (Dodoma), Ujenzi wa Stendi Mpya Mabasi Mbulu, Ujenzi wa barabara za lami, mitaro na taa za barabarani, kuboresha miundombinu ya dampo Busoka, Kuboresha miundo mbinu ya Masoko ya Sango, Kagongwa, Majengo, Mayila na Namanga na kuendelea na maandalizi ya Mpango Kabambe wa Halmashauri ya Mji wa Kahama (Master Plan) kupitia fedha za Benki ya Dunia .
- Kutenga fedha kwa ajili ya mikopo ya wanawake, Vijana na wenye ulemavu
- Kuimarisha usafi na mazingira kwa kuimarisha ;
- Uboreshaji wa maslahi ya watumishi kwa upandishwaji wa madaraja na kubadilishiwa miundo yao ya kazi, kulipa haki na stahili zao kwa wakati mfano, matibabu, likizo, mishahara nk.
- Hifadhi ya Mazingira, Udhibiti wa UKIMWI, Lishe, Ulinzi wa mama na mtoto, Udhibiti wa Rushwa. Suala Uchaguzi Mkuu pia limeangaliwa katika Bajeti hii pamoja na uhuishaji wa Mpango Mkakati wa Halmashauri wa 2016/17- 2021/22.

1. Ili kutekeleza vipaumbele vilivyoainishwa hapo juu Halmashauri inatarajia kukusanya na kutumia jumla ya Tsh. **40,900,324,703.00** kwa mgawanyo ufuatao:-

| | | |
|---|---|---|
| -Mapato ya Ndani | - Tsh. | 6,579,322,750.00 |
| -Mishahara | -Tsh. | 27,144,006,000.00 |
| -Matumizi ya Kawaida | -Tsh | 1,014,598,000.00 |
| -Miradi ya Maendeleo | -Tsh | 4,676,734,953.00 |
| -Elimu Bila Malipo | - Tsh | 1,485,663,000.00 |
| **JUMLA KUU** | -Tsh | **40,900,324,703.00** |

Makadirio ya Bajeti kwa mwaka huu yameongezeka kwa wastani wa asilimia 8.0 ikilinganishwa na mwaka 2020/21. Ongezeko hili limetokana na
eneo la mishahara kwa sababu ya watumishi watakaopandishwa madaraja na ajira mpya.

## 4.0 MIKAKATI

Ili kufikia malengo tuliyojiwekea na kwa kuzingatia changamoto zilizopo tunatarajia kuboresha ukusanyaji wa Mapato ya ndani kwa utekelezaji wa Bajeti Mwaka wa Fedha 2021/22 kwa kutumia mikakati ifuatayo:

**a) Mikakati ya Ukusanyaji wa Mapato**

1. Kuongeza uwazi na uwajibikaji wa matumizi ya Kodi, Tozo, Ada na Ushuru kwa wananchi.
2. Kufanya utambuzi wa vyanzo vya mapato vyote vilivyoko katika Halmashauri (Revenue enhancement).
3. Kuendelea kutoa elimu kwa wananchi juu ya umuhimu wa ulipaji kodi kwa wakati.
4. Kuchukua hatua za kisheria kwa wakwepaji wa Kodi.
5. Kupanua wigo wa mapato kwa kuboresha vyanzo vya mapato vilivyopo na kuanzisha vingine (ukamilishaji wa miundombinu masoko Sango, Majengo, Malunga, Kazaroho na stendi za Kagongwa na Mbulu(Nyasubi) na kuimarisha miundombinu eneo la viwanda vidogo, kati na vikubwa Bukondamoyo (Dodoma))
6. Kupitia upya viwango vya ada, ushuru na kodi na hatimae kuboresha sheria ndogo za Halmashauri.
7. Usimamizi na ufuatiliaji wa mapato ya ndani kusimmamiwa kwa karibu na Timu ya Mapato ya Halmashauri ambayo tayari imekwishaundwa.
8. Kuimarisha usafiri kwa wakusanya mapato kwa kununua gari kwa ajili ya ukunyaji mapato.

**b) Mikakati ya utekelezaji wa Bajeti**

1. Kupanua wigo wa mapato kwa kuboresha vyanzo vya mapato vilivyopo na kuanzisha vingine (ukamilishaji wa miundombinu masoko Sango, Kazaroho na stendi za Kagongwa na Mbulu(Mhongolo) na kuimarisha miundombinu eneo la

viwanda vidogo, kati na vikubwa Bukondamoyo (Dodoma) ili kupata fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi , uendeshaji wa ofisi na malipo ya stahili za watumishi.

2. Kujaza nafasi zenye mapungufu ya watumishi hasa katika sekta za Ujenzi, Afya na Fedha na Biashara kwa kutenga bajeti ya mishahara katika maeneo hayo.

3. kubadilishiwa miundo yao ya kazi kwa watumishi wanashili katika kada zenye mapungufu.

4. Kuendelea kutoa elimu juu ya sheria na taratibu za manunuzi ngazi za Msingi na kwa Wakuu wa Idara.

Baada ya kuangalia na vipaumbele na mikakati ya utekelezaji wa Mpango na Bajeti 2021/22 naomba kuwasilisha jedwali la Umbile la Bajeti kwa Vyanzo vya Mapato ya Ndani, Ruzuku na Wahisani kama inayoonekana hapa chini:

**JEDWALI LA UMBILE LA BAJETI 2021/2022**

| IDARA/ KITENGO | BAJETI 2020/2021 |
|---|---|
| **A-MAPATO** | |
| I: a.Vyanzo vya ndani-Proper | 5,478,023,000.00 |
| b. Vyanzo Kingwa (CHF, NHIF, USER FEE, ADA MASHULENI) | 1,101,299,750.00 |
| **Jumla Mapato ya Ndani** | **6,579,322,750.00** |
| II: **Ruzuku toka Serikali** | |
| **Matumizi ya Kawaida** | |
| Kilimo/ushirika | 5,476,480.00 |
| Mifugo na Uvuvi | 3,080,520.00 |
| Elimu Msingi | 57,967,000.00 |
| Elimu Sekondari | 30,645,000.00 |
| Afya | 138,526,000.00 |
| Ujenzi | 14,921,000.00 |
| Maji | 0.00 |
| **Jumla ndogo** | **250,616,000.00** |
| **Matumizi Mengineyo Idara za Utawala**: | |
| Utawala | 0 |
| Mkaguzi wa Ndani | 3,182,580.00 |
| Fedha na Biashara | 0 |
| Mipango, Takwimu na Ufuatiliaji | 11,516,580.00 |
| M/Jamii | 2,652,150.00 |
| Nyuki | 0 |
| Usafi na Mazingira | 1,768,100.00 |
| Ardhi na Mipango Miji | 2,828,960.00 |
| Uchaguzi | 4,006,630.00 |
| **Jumla Ndogo Idara za Utawala** | **25,955,000.00** |
| **Fidia ya Vyanzo** | |
| Utawala | 42,208,000.00 |
| **Jumla Ndogo Fidia ya Vyanzo** | **42,208,000.00** |

| IDARA/ KITENGO | BAJETI 2020/2021 |
|---|---|
| **Mitihani** | |
| Shule za Msingi | 171,790,000.00 |
| Shule za Sekondari | 192,886,000.00 |
| **Jumla Ndogo Mitihani** | **364,676,000.00** |
| **Uhamisho- Elimu** | |
| Shule za Msingi | 42,698,000.00 |
| Shule za Sekondari | 28,538,000.00 |
| **Jumla Ndogo Uhamisho** | **71,236,000.00** |
| **Likizo- Elimu** | |
| Shule za Msingi | 120,396,000.00 |
| Shule za Sekondari | 36,078,000.00 |
| **Jumla Ndogo Likizo** | **156,474,000.00** |
| **Afya** | |
| Posho ya wito( On call allowance) | 103,433,000.00 |
| **Jumla Ndogo Posho ya Wito** | **103,433,000.00** |
| **Jumla Matumizi ya Kawaida na Fidia ya vyanzo vya** | **1,014,598,000.00** |
| III:**Mishahara** | |
| Mishahara | 27,144,006,000.00 |
| **Jumla ndogo** | **27,144,006,000.00** |
| | |
| **IV-Miradi ya Maendeleo(Ruzuku na Wahisani)** | |
| RBF | 880,689,564.00 |
| SEDP | 242,680,000.00 |
| TASAF III | 2,174,030,354.00 |
| IMMA (AFYA) | 79,990,000.00 |
| WORLD VISION (AFYA) | 263,649,847.00 |
| Mfuko wa Afya-Basket fund | 485,204,553.00 |
| Mfuko wa Jimbo (CDF) | 54,145,000.00 |
| UNICEF | 5,733,000.00 |
| AGPAH | 393,966,635.00 |
| Global Fund | 16,656,000.00 |
| Inter church Medical Assistance | 79,990,000.00 |
| **Jumla ya Miradi Ruzuku na Wahisani** | **4,676,734,953.00** |
| | |
| **V: Elimu bila Malipo** | |
| Elimu Bila Malipo | 1,485,663,000.00 |
| **Jumla ndogo Elimu Bila Malipo** | **1,485,663,000.00** |
| **JUMLA KUU MAPATO I-V** | **40,900,324,703.00** |
| | |
| **B-MATUMIZI** | |
| I. Vyanzo vya ndani | |
| Matumizi ya Kawaida | 2,168,745,200.00 |
| Miradi ya Maendeleo | 3,286,813,800.00 |
| Mishahara | 22,464,000.00 |
| Vyanzo Lindwa (CHF, NHIF, USER FEE, ADA MASHULENI) | 1,101,299,750.00 |
| **Jumla Mapato ya Ndani** | **6,579,322,750.00** |

| IDARA/ KITENGO | BAJETI 2020/2021 |
|---|---|
| II.Maeneo yanayopata Ruzuku | |
| Mishahara | 27,144,006,000.00 |
| Matumizi ya kawaida | 1,014,598,000.00 |
| Miradi ya maendeleo | 4,676,734,953.00 |
| Elimu Bila Malipo | 1,485,663,000.00 |
| **Jumla Maeneo ya Ruzuku** | **34,321,001,953.00** |
| **JUMLA YA MATUMIZI YOTE I-II** | **40,900,324,703.00** |

Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Miradi ya Maendeleo kwa sekta za vipaumbele unafafanuliwa kwa kifupi kama ifuatavyo:

## I. Sekta za kiuchumi

a) Kilimo, Umwagiliaji na Ushirika.

Ili kuhakikisha wananchi wanapata huduma za ugani za kilimo Halmashauri kwa mwaka 2021/22 imepanga kununua pikipiki kwa Maafisa Ugani katika kata za Kinaga, Ngogwa, Zongomela na Isagehe. Upatikanaji wa mbegu zinazostahili ukame na ruzuku za pembejeo za kilimo kwa wakulima 345 limefanyiwa kazi pia katika bajeti hii. Suala jingine ni ukrabati wa mradi wa umwagiliaji Lowa ili kuwazesha wakulima wa bustani na mbogamboga kulima wakati wote wa mwaka na tija. Kupitia wadau wa Maendeleo mradi wa viazi lishe na maharage utatekelezwa na World Vision kata ya Kilago, Iyenze, Mhongolo, Mondo, Mwendakulima, Kagongwa, Isagehe, Nyendekwa, Zongomela na Busoka. Vilevile Halmashauri kupitia wadau itaanzisha vitalu vya miche ya maembe (bolibo na dodo) kwa ajili ya kusambaza miche hii kwa wananchi ili malighafi ya viwanda vya juisi vinavyoendelezwa na wadau wetu wa maendeleo eneo la Chapulwa, Bukondamoyo na Mwendakulima.

b) Mifugo na Uvuvi

Ili kuhakikisha wananchi wanapata huduma za ugani za Mifugo na Uvuvi Halmashauri kwa mwaka 2021/22 imepanga kukarabati machinjio ya kuchinjia wanyama ya Busoka na Kagongwa,ukarabati wa majosho 2 katika kata ya Kinaga na Mondo,miradi mingine ni kuingiza mfumo wa maji katika machinjio ya Kagongwa,kujenga vizimba vya kuuzia ng’ombe kwenye mnada wa Ngogwa,kutoa chanjo kwa mifugo katika kata 20 za Kahama

mji,kuhamilisha mifugo ili kupata kosafu bora katika kata 20 za Kahama Mji,Kuwa na kituo cha kukusanya na kupima ubora wa maziwa Kahama mjini. Kupitia wadau wa Maendeleo mradi wa mbuzi wa maziwa unatekelezwa na World Vision kata ya Kilago, Iyenze, Mhongolo, Mondo, Mwendakulima, Kagongwa, Isagehe, Nyandekwa , Zongomela na Busoka. Vilevile Farm concern wanatoa elimu za ugani za ufugaji kuku na samaki kwa wananchi wa Mondo na mwendakulima. Shughuli nyingine itakayofanyika ni kuwa shamba darasa la ufugaji samaki eneo la Mwendakulima ili kutoa elimu ya ufugaji wa samaki kwa ajili ya kuboresha kipato na lishe.

c) Ujenzi

Halmashauri kupitia Idara ya Ujenzi inalo jukumu kubwa la usimamizi na ufuatiliaji wa miradi yote ya Halmashauri. Kwa mwaka wa Fedha 2021/2022, utekelezaji wa miradi ni pamoja na kuwezesha ukuaji wa mazingira ya kibiashara katika maeneo ya uwekezaji mapato /eneo la viwanda Bukondamoyo/eneo la stendi Kagongwa na masoko ya Namanga, Sango, Soko kuu, Malunga, Mayila, Magwanji, Nyahanga na Majengo. Pamoja na Halmashauri imepanga kuboresha miundombinu kwenye maeneo ya uwekezaji ya stendi za Majengo, CDT, Bukondamoyo, Mbulu pamoja na masoko ikiwa ni pamoja na kujenga mitaro ya maji ya mvua.

d) Maendeleo ya Jamii

Halmashauri inatarajia kutoa mikopo ya Wanawake , Vijana na Wenye Ulemavu kiasi cha Tsh. 574,613,300.00 kwa Mwaka 2021/22. Aidha Kiasi cha Tsh. 23,532,700.00 kitatumika kuandaa mazingira wezeshi kwa vijana na wanawake eneo la viwanda Bukondamoyo na Kagongwa. Suala la elimu ya ujasiriamali kupitia kituo chetu cha uwezeshaji wananchi kuuchumi limeangaliwa katika mapango na bajeti hii.

## II. Sekta za utoaji huduma

a) Elimu Msingi

Halmashauri ina jumla ya shule za Msingi za Serikali 79 zenye jumla ya wanafunzi 83,475 wa madarasa ya Awali hadi la saba Mwaka 2020. Kutokana na idadi hiyo ya Wanafunzi na Walimu imeongeza changamoto ya Miundombinu na kuwa na upungufu wa madarasa 1089 kati ya 1855 yanayohitajika, upungufu wa matundu ya vyoo 2805 kati ya 3657 yanayohitajika, upungufu wa nyumba za walimu 1755 kati ya 1855 zinzohitajika na upungufu wa madawati 7,829 kati ya 27825 yanayohitajika. Katika kukabiliana na changamoto za upungufu wa miundombinu tajwa hapo juu, Halmashauri imejipanga kukamilisha vyumba vya Madarasa 102 , madawati 1530, Matundu ya vyoo 150 na kukamilisha na kukarabati Nyumba 5 za Walimu toka vyanzo mbalimbali vya fedha zikiwemo nguvu za Wananchi.

b) Elimu Sekondari

Halmashauri ina jumla ya Wanafunzi 12,468 ( Wav- 5,969 na Was- 6,499) na Walimu 468 katika Idara ya Elimu Sekondari. Kutokana na idadi hiyo ya Wanafunzi na Walimu imeongeza changamoto ya Miundombinu na kuwa na upungufu wa madarasa 133 kati ya 357 yanayohitajika, upungufu wa matundu ya vyoo 363 kati ya 586 yanayohitajika, nyumba za walimu 406 kati ya 468 na upungufu wa viti na meza 5,432 kati ya 16,068 vinavyohitajika. Katika kukabiliana na changamoto za upungufu wa miundombinu tajwa hapo juu, Halmashauri imejipanga kukamilisha vyumba vya Madarasa 51 , viti na meza 979, Matundu ya vyoo 117, ujenzi wa uzio na kukamilisha na kukarabati Nyumba 4 za Walimu toka vyanzo mbalimbali vya fedha zikiwemo nguvu za Wananchi.

c) Afya na Ustawi wa Jamii

Kwa mwaka wa fedha 2021/2022 Halmshauri imepanga kuviwezesha vituo vipya kupata vifaa Tiba ili viweze kutoa huduma bora za Afya kwa wananchi.Hata hivyo ipo mikakati ya Jumla ya Halmashauri Idara ya Afya ni:

- Kuendelea kuhamasisha wananchi kujiunga Bima za Afya ikiwemo CHF, NHIF na Bima zingine ili kuhakikisha upatikanaji wa dawa na vifaa tiba katika vituo vya kutolea huduma za afya zinapatikana kwa kiwango kinachotakiwa.
- Kutenga Tsh. 1,000.00 kwa watoto 48,787 walioko chini ya umri wa miaka 5 kwa ajili ya huduma za afya na Lishe.
- Kuimarisha Mifumo ya makusanyo katika vituo vyote vya kutolea huduma za Afya
- Kuimarisha miundo mbinu yote katika vituo vyote vya serikali katika Halmashauri ya Mji . Halmashauri itaendelea na ukamilishaji wa jengo la wagonjwa wa nje (OPD) , Kituo cha Afya Nyasubi, Zahanati ya Chapulwa, Wendele, Ngulu na ujenzi wa wodi ya wazazi pamoja na chumba cha upasuaji Kituo cha Afya Mwendakulima.
- Kuendelea kutambua wananchi wenye vigezo walio katika makundi maalum na kuwapatia vitambulisho vya Bima ya Afya ya Jamii ili kuweza kuapata huduma za Afya bila malipo. Wazee 3000 wanatarajiwa kupewa vitambulisho vya matibabu kwa mwaka 2021/2022.
- Kutengeneza Mpango wa ajira za muda kwa watumishi wa Afya katika fani mbalimbali ikiwemo watumishi wanaofanya kazi kwa kujitolea.
- Kiasi cha Tsh. 11,000,000.00 kimetengwa kwa ajili ya kuzuia ukatili dhidi ya wanawake na watoto na kusimamia kamati za ukatili dhidi ya wanawake na watoto katika ngazi ya Halamshauri, Kata na Vijiji. Suala la watoto waishio katika mazingira magumu limezingatiwa pia katika bajeti hii kwa kuwatengea fedha za kuwaunganisha na familia zao na kuwalipia ada wasiokuwa na uwezo.
- Kuweka kwenye Mpango ukarabati wa Miundo mbinu ikiwemo Wodi za wagonjwa.

  Pamoja na ufafanuzi huu mfupi kisekta nimeambatisha majedwali yanayoonyesha miradi iliyotekelezwa Mwaka 2019/2020, nyanzo mbalimbali vya Mapato ya Ndani kwa Mwaka 2021/2022 na michanganuo ya bajeti za matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo kwa sekta na vitengo vya Halmashauri.

## MWISHO

Bajeti ya 2021/2022 ni mwendelezo wa jitihada za Halmashauri katika kufikia Malengo ya Mpango wa II wa Maendeleo, Mpango Mkakati wa Halmashauri, Mpango wa Maendeleo Endelevu na hatimaye Dira ya Maendeleo 2025. Hata hivyo ili kufikia malengo yetu mapema, kila mdau anapaswa kuwajibika na kushiriki kikamilifu ili kufikia adhima ya Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa John Joseph Pombe Magufuli ya kauli mbiu ya “**HAPA KAZI TU**”.